

Siku niliyo ondoka nyumbani
kuelekea jijini!



Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Siku niliyo ondoka nyumbani kuelekea
jijini!

Written by: Lesley Koyi, Ursula Nafula

Illustrated by: Brian Wambi

Translated by: Ursula Nafula

This story originates from the African Storybook
(africanstorybook.org) and is brought to you by
Storybooks Canada in an effort to provide
children's stories in Canada's many languages.




This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0).
<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>

✎ Lesley Koyi, Ursula Nafula
👤 Brian Wambi
📖 Ursula Nafula
😊 Kiswahili
📖 Level 3


(imageless edition)







Kituo kidogo cha mabasi kijijini mwetu kilijaa shughuli za watu na mabasi. Basi nyingi zilikuwa zimejaza mizigo. Chini, palikuwa na mizigo zaidi ya kupakia. Kondakta waliita majina tofauti ya mahali basi zilielekea.

“kwenda jijini! kwenda jijini! kwenda
magharibi!” Nilisikia kondakta akita kwa
sauti. Ie ndiyo basi niliyohitaji kupanda
kwa usafiri wangu.






Basi la kwenda jijini lilikuwa karibu kujaa, lakini watu zaidi walijishughulisha kutaka kupanda. Baadhi yao walipakia mizigo chini ya basi. Wengine waliweka katika sehemu ya juu.





Basi la kurudi lilikuwa linajaa upesi. Muda mfupi baadaye, lingeanza safari ya kwenda mashariki. Jambo la maana kwangu wakati huo lilikuwa kuanza kutafuta nyumba ya mjomba wangu.

Abiria wapya walishika tiketi zao huku
wakitafuta mahali pa kuka. Wanawake
waliokuwa na watoto wodogo
waliwatayarisha kwa safari hiyo ndefu.




Bada ya saa tisa, niliamshwa kwa kelele
za kita abiria waliokwenda katika kijiji!
chang. Nilichukwa mfuko wangu
mdogo na kuruka nje ya basi.





Nilipenyeza ndani nikakaa karibu na dirisha. Mtu aliyeketi karibu nami alishika mfuko wa plastiki wa kijani kibichi. Alivaa viatu vilivyozeeka, koti kukuu na alionekana kuwa na wasiwasi.




Njiani, nilikariri jina la mahali mjomba wangu alipoishi katika jiji kubwa. Nilikuwa bado nafikiria wakati nilipopatwa na usingizi.

Lakini mawazo yangu yalirejea nyumbani.
Je, mamangu atakuwa salama? Je, sungura
wangu wataleta hela zozote? Je, ndugu
yangu atakumbuka kunyunyizia maji
miche ya miti yangu?


14

Niliangalia nje na kutambua kwamba
nilikuwa naondoka kijijini mwangu, mahali
ambapo nililelewa. Nilikuwa naenda katika
jiji kubwa.


7




Upakiaji mizigo ulikamilika na abiria wakawa wameketi. Wachuuzi walizidi kusukumana kutaka kuingia ndani ya basi ili wauze bidhaa zao. Kila mmoja alitaja kwa sauti majina ya bidhaa alivyokuwa anauza. Maneno yao yalinifurahisha.




Safari ilipoendelea, joto lilikuwa jingi ndani ya basi. Niliyafumba macho yangu nikuuia kulala.




Baadhhi ya abiria walinnua vinywaji.
Wengine wakanunua vitafunwa vidogo na
kuanza kutafuna. Wasiokuwa na fedha,
kama mimi, walitazama tu.



Basi lilipoondoka kituoni, nilichungulia
dirishani. Nilijuliza endapo ningerudi na
kwenda kijijini kwangu tena.



Shughuli hizi zilikatizwa kwa mlio wa honi ya basi, ishara kwamba tulikuwa tayari kuondoka. Kondakta aliwataka wachuuzi kuondoka ndani ya basi.



Wachuuzi walisukumana huku wakitafuta njia ya kushuka. Wengine wao waliwarudisha abiria chenji zao. Wengine walifanya juhudi za mwisho kuuza bidhaa zao.